TANGAZO LA SERIKALI Na. 810 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NYANGH'OMANGO II YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Nyangh'omango II ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

---

JEDWALI

---

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV528 yenye majira-nukta 479219MS, 9671394KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ308$^{0}$32'00"MS kwa umbali wa kilomita 5.512 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV531 yenye majira - nukta 483391MS, 9667998KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS36$^{0}$07'00"KS kwa umbali wa kilomita 3.694 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV514 yenye majira-nukta 481299MS, 9665045KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Ksini - Mashariki katika uelekeo wa KS318$^{0}$04'00"MS kwa umbali wa kilomita 2.664 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV495 yenye majira - nukta 483063MS, 9663076KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS27$^{0}$00'00''KS kwa umbali wa kilomita 3.212 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV543 yenye majira-nukta 481668MS, 9660123KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kuskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS114$^{0}$ 52' 00''MG kwa umbali wa kilomita 2.524 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV510 yenye majira - nukta 476703MS, 9662406KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ114$^{0}$ 52' 00" MG kwa umbali wa kilomita 1.269; baada ya hapo mpaka unafuata bonde linaloteganisha Mkoa wa Geita na Wilaya ya Misungwi hadi Ziwa Victoria; baada ya hapo mpaka unafuata mwambao wa ziwa Victoria hadi ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*